# Uhifadhi Endelevu wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania

## Simulizi Kutoka katika Miradi ya Jamii











Mei

2018

EASTERN ARC MOUNTAINS CONSERVATION ENDOWMENT FUND

EAMCEF

MFUKO WA HIFADHI YA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI

“Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sana sote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadae. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu. Uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yote yenye mapori huhitaji maarifa ya kitaalamu, wafanyakazi waliopata mafunzo maalumu, na fedha; na hivyo tunaomba mataifa mengine yashiriki nasi katika kazi hii muhimu, ambayo kufanikiwa ama kutofanikiwa kwake hakuathiri tu Bara la Afrika bali ulimwengu mzima kwa ujumla”

**Mwalimu Julius K. Nyerere, Septemba 1961**

# YALIYOMO


01 Dibaji

02 Eneo la Mradi

03 Uwiano katika Uhifadhi: Kula kuku badala ya nyamapori ili kuokoa misitu

07 Ufugaji vipepeo – Ni ajabu!

11 Ufugaji nguruwe kwa manufaa mbalimbali

15 Ufugaji mbuzi wa maziwa ni tofauti na mazoea!

18 Kama mazao ya kilimo hayatabadilisha maisha yetu, ng’ombe wa maziwa watayabadilisha

23 Jinsi upandaji miti unavyopindua umaskini katika Wilaya ya Kilolo

28 Kama isingekuwa ufugaji nyuki…

30 Malipo ya ahadi ya kuhifadhi msitu

34 Kuokoa misitu kwa kupambana na hali ya ukosefu wa chakula

36 Kufidia nguvu na muda kwa wanaja

39 Utengenezaji wa majiko bora yenye manufaa kwa wanawake na misitu




# DIBAJI

Kupitia ufadhili wa fedha kutoka Ubalozi wa Ufalme wa Norway uliopo Dar -es-Salaam, Taasisi ya Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (yaani EAMCEF) imetekeleza kwa ukamilifu mradi wa miaka mitano (Juni 2011-Mei 2016) wa "Kuboresha uhifadhi wa misitu ya milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania" uliolenga maeneo ya Hifadhi za Asilia tisa ambazo ni; Amani, Nilo, Chome, Magamba, Mkingu, Uluguru, Kilombero na Uzungwa Scarp na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa. Utekelezaji wa mradi ulifanyika kupitia washirika waliopo katika Halimashauri za Wilaya kumi na moja zilizopewa kipaumbele katika mradi na ambazo zinaguswa na maeneo hayo ya Hifadhi, Wilaya hizo ni - Muheza, Korogwe, Mkinga, Same, Lushoto, Mvomero, Morogoro, Manisipaa ya Morogoro, Kilombero, Kilolo na Mufindi.

Wadau wa mradi waliratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za mradi katika eneo la mradi, EAMCEF ilitoa ruzuku za kuwezesha utekelezaji wa miradi midogomidogo katika maeneo makuu matatu - uhifadhi na usimamizi wa misitu; maendeleo ya jamii na uboreshaji wa shughuli za kujikimu, na tafiti za bioanuwai na mabadiliko ya tabianchi. Wakati utekelezaji wa miradi ya uhifadhi na usimamia wa misitu ililenga katika kuhifadhi kikamilifu bioanuwai na kuboresha hali ya misitu katika kila eneo la maeneo tisa ya kipaumbele, miradi ya maendeleo ya jamii na uboreshaji wa shughuli za kujikimu ulilenga katika kuboresha hali za kiuchumi na kijamii za jamii zinazoishi pembezoni mwa maeneo lengwa ya Hifadhi kwa kuwezesha utekelezaji wa njia mbadala za shughuli za kujikimu. Miradi ya tafiti za bioanuwai na mabadiliko ya tabianchi ilitekelezwa ili kutoa taarifa muhimu zinazosaidia katika ufanyaji maamuzi na upangaji wa mipango pamoja na uhifadhi madhubuti wa maeneo ya misitu lengwa.

Kutokana na kukamilisha kwa ukamilifu mradi mwezi Mei 2016, Mfuko ulianzisha mchakato wa kuweka kumbukumbu za matokeo na manufaa yaliyotokana na utekelezaji wa mradi ili kuelezea maendeleo, kushirikishana uzoefu uliopatikana, mambo ya kujifunza na mbinu bora za kuigwa zilizotumika katika utekelezaji wa mradi. Kisha, mwishoni mwa mwaka 2017 maeneo husika yalitembelewa na waandaji wa simulizi zilizomo katika makala hii ambazo zilisimuliwa na wanufaika wa mradi kutoka katika maeneo machache yaliyoteuliwa kuwakilisha mengine. Ni matumaini yetu kwamba simulizi hizi zitakuvutia na zitakuwa zenye kukufaa.

**Francis B.N. Sabuni**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Morogoro, Tanzania**

**Mei, 2018**

# MIRADI YETU

## MAENEO MAKUU


**146** — **Miradi ya usimamizi shirikishi na maendeleo ya jamii**

**40** — **Miradi ya Maeneo ya Hifadhi na Mabadiliko ya Tabianchi**

**18** — **Miradi ya tafiti za Bioanuwai na Mabadiliko ya Tabianchi**

Simulizi zilizomo katika kitabu hiki zinajikita katika Miradi ya usimamizi shirikishi na Maendeleo ya jamii

# MAENEO YA UTEKELEZAJI WA MRADI




| | | |
|---|---|---|
| 1 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Chome | Wilaya ya Same |
| 2 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Magamba | Wilaya za Lushoto na Korogwe |
| 3 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani | Wilaya za Muheza na Korogwe |
| 4 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Nilo | Wilaya za Mkinga, Muheza na Korogwe |
| 5 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu | Wilaya ya Mvomero |
| 6 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Uluguru | Wilaya za Mvomero na Morogoro na Manispaa ya Morogoro |
| 7 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Kilombero | Wilaya za Kilombero na Kilolo |
| 8 | Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Uzungwa Scarp | Wilaya za Kilolo, Mufindi na Kilombero |
| 9 | Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa Scarp | Wilaya za Kilolo na Kilombero |



# Uwiano katika Uhifadhi: Kula kuku badala ya nyamapori ili kuokoa misitu

**Kijiji cha Mkanga, Wilaya ya Mvomero**
**Msitu uliopo jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu**

Kama ilivyo katika maeneo mengine ya Misitu ya Hifadhi wakazi wa kijiji cha Mkanga wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mkingu wameendelea kutegemea misitu iliyopo jirani nao ili kukidhi mahitaji yao ya nyamapori kama chanzo kikuu cha protini.

Kwa kawaida ili kujipatia nyamapori wanakijiji huingia msituni na kuwinda wanyama wadogowadogo hasa aina ya Ndezi (wanaofahamika kwa Kiingereza kama Cane rats). Pamoja na kwamba Ndezi ni wanyama wadogo wenye uzito kati ya kilo 6 mpaka 10, nyama ya Ndezi inapendwa zaidi kutokana na ulaini wake na ladha tamu kuliko ile ya kuku wa kienyeji. Ili kufanya zoezi la kuwinda kuwa rahisi, wawindaji hawawindi kwa kutumia mbwa tu bali pia huchoma nyasi kuwatisha Ndezi ili wawakimbize kwa urahisi. Ni uchomaji huu wa nyasi ndio husababisha miotopori yenye kuharibu misitu ya thamani na bioanuwai za msituni na kuacha misitu ikiwa imeharibika.

Ili kushughulikia changamoto hii, mwaka 2013, EAMCEF ilitoa ruzuku ya kuanzisha ufugaji wa kuku bora wa kienyeji, kutoa mafunzo na mbinu kwa kikundi cha watu 25 katika kila kijiji. Jambo la kuvutia sana katika ufugaji huu wa kuku lilikuwa ni uanzishwaji wa vifaa maalum vya kienyeji vya kukuzia vifaranga kwa lugha ya asili vinaitwa Vinengunengu (yaani kwa Kiingereza chick brooders). Kwa kuanzia, EAMCEF ilisaidia utoaji wa mtaji wa kuku majike wa 5 na jogoo moja kwa kila mshiriki wa mafunzo. EAMCEF iliamini kwamba kuku wa kienyeji watakuwa mbadala wa Ndezi na hivyo kuiokoa misitu kutoka kwenye janga la uchomaji moto. Tangu wakati huo wanakijiji wameshuhudia matokeo makubwa katika uzalishaji wa mayai na kuku. Matumizi ya Vinengunengu yamesaidia wafugaji kuwa na uhakika wa kufuga hadi vifaranga 248 vinavyotokana na kuku mmoja kwa mwaka. Ongezeko la uzalishaji limewezesha upatikanaji wa protini (nyama na mayai) katika ngazi za kaya na kijiji na hivyo kupunguza matukio ya kuchoma misitu.

**Ni ufugaji wa kuku ndio umebadilisha maisha ya wanakijiji wanaoshiriki katika ufugaji. Mapato yatokanayo na uuzwaji wa kuku na mayai yamekuwa yakitumika kugharimia mahitaji ya kaya na muhimu zaidi yamegharimia mahitaji makubwa kama vile ada za shule, huduma za afya, ukarabati wa nyumba, ujenzi wa nyumba za kisasa na ujenzi wa vyoo bora.**



**Baadhi ya wanakijiji wametumia mapato yatokanayo na mauzo ya kuku na mayai katika:**

- Kuweka mitambo ya umeme wa sola na kuangaza nyumba zao na kuwezesha wanafunzi kupata muda wa ziada wa kujisomea nyumbani na hivyo kuboresha ufaulu wao kwa ujumla
- Kupanua shughuli za kilimo kwa kununua maeneo mengine ya ardhi, kuajiri vibarua, hivyo kuchangia katika ongezeko la uzalishaji na upatikanaji imara/usalama wa chakula
- Kununua ng'ombe wa maziwa na kuwa na uhakika wa maziwa ya kutosha na mbolea kwa ajili ya shughuli za kilimo cha bustani

## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka katika maeneo ya mradi- Wilaya za Korogwe, Same na Mvomero

- **Watu 873 (wanawake 535: wanaume 338)** walipewa mafunzo ya ufugaji na utunzaji bora wa kuku
- **Kuku bora 2,061** walisambazwa kwa wanavijiji
- **Kaya 439** zilipatiwa kuku bora
- **Mapato ya ShT. 17,420,500** yalitokana na mauzo ya mayai
- **Mapato ya ShT. 26,766,600** yalitokana na mauzo ya vifaranga
- **Mapato ya ShT 38,858,000** yalitokana na mauzo ya kuku
- **Kilo 13,760 za samadi** itokanayo na kuku zilitumika katika kilimo cha bustani za nyumbani.




### ROHAN BELINGTON MANGA

Kwa miaka mitatu iliyopita kuku (akimaanisha mapato yanatokana na mauzo ya kuku) wamekuwa wakilipa ada za shule za watoto wangu, mmoja wa wanangu alifanikiwa kujiunga na chuo na sasa ameajiriwa. Tunaheshimika sana hapa kijijini kwetu kwa sababu tu ya kuku, sasa tunatimiza vigezo vinavyotuwezesha kupata mkopo kutoka katika VICOBA kwa ajili ya shughuli nyingine za ujasiriamali. Sitegemei tena kurudi msituni kwa ajili ya kuwinda Ndezi kwa sababu sasa kuna nyama ya kutosha [kuku] inayopatikana katika jamii haswa katika mji wangu.



### PETER FELIX MBUYA

Mwaka 2017 pekee nimepata zaidi ya ShT 700,000 kutokana na mauzo ya mayai na kuku, nilitumia kiasi fulani cha fedha kununua ng'ombe wa maziwa.... jambo hili lisingewezekana kama isingalikuwa ufugaji wa kuku. Kuku wananiwezesha kutimiza mahitaji yangu ya kifedha bila kuomba msaada kwa ndugu au majirani.



### AMANI B. MTASIWA

Kabla ya kujiunga na mradi huu, chanzo changu kikuu cha kipato kilitokana na ufanyaji wa kibarua katika mashamba ya watu wengine lakini kipato kilikuwa ni kidogo sana na kisichopatikana kwa muda mwafaka. Kwa sasa, kwa kuuza mayai na kuku nimeweza kununua shamba langu mwenyewe, nimenunua pampu ya maji kwa ajili ya bustani yangu na kwa sasa ninaweza kuilisha familia yangu katika kipindi cha mwaka mzima. Kupitia kuku hawa nimeweza kukusanya baadhi ya fedha na kuamua kujenga nyumba bora, iliyoezekwa kwa bati na ambayo inaifanya familia yangu kuwa na furaha.



### BERNADETHA BASIL OISSO

Kama isingalikuwa kuku nisingeweza kumudu matibabu yangu ya moyo huko Dar es Salaam, kuku wameokoa maisha yangu. Kabla ya kufuga kuku nilikuwa naweza kulima ekari moja tu lakini sasa naweza kuajiri vibarua na kulima hadi ekari nne.





NYUMBA YA ZAMANI



NYUMBA MPYA

"Kupitia kuku hawa nimeweza kukusanya fedha na kuamua kujenga nyumba bora,iliyoezekwa kwa bati na ambayo inaifanya familia yangu kuwa yenye furaha"

**(Amani B. Mtasiwa, Kijiji cha Mkanga, Wilaya ya Mvomero)**



# Ufugaji vipepeo – Ni ajabu!

**Kijiji cha Bwambo, Wilaya ya Same**
**Msitu uliopo jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Msitu wa Chome**



## TAKWIMU MUHIMU

Wilaya ya Same kwa Ujumla

- **Wanakijiji 396 (wanawake 180: wanaume 216) walipewa** mafunzo ya ufugaji wa vipepeo katika Wilaya ya Same
- **Kaya 72** zinajihusisha na ufugaji wa vipepeo
- **Mabuu 1,400** walifugwa mwaka 2017
- **Mabuu 1,200** waliuzwa mwaka 2017
- **ShT 2,760,000** zilipatikana kutokana na uuzaji wa mabuu

"Mradi wa kufuga vipepeo ulipoanzishwa katika kijiji chetu watu walikuwa wanache ka na kuuchukulia kama kitu cha kipumbavu pumbavu hivi… ni jambo la kuaibishakuona mtu mzima akizunguka na kukamata vipepeo" alieleza Msese E. Elifuraha wa kijiji cha Bwambo kilichopo katika Wilaya ya Same. Mzee Elifuraha na wenzake wanaounda Kikundi cha Ufugaji wa Vipepeo wanafuraha kujithibitishia kwamba mradi wa ufugaji vipepeo ni rahisi na kiuchumi ni njia ya kupata mapato mbadala - na hauna hekaheka!

EAMCEF ilianzisha mradi wa ufugaji vipepeo ili kusaidia wanajamii kuutumia mradi huo kama njia mbadala ya kujipatia kipato na kama mkakati wa kupunguza utegemezi mkubwa wa misituyaani Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Msitu wa Chome.

Wanakikundi cha Ufugaji Vipepeo walipewa mafunzo na kutembelea moja ya eneo la kutunzia vipepeo katika Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Msitu wa Amani kwa ajili ya kujifunza zaidi. Waliporudi kutoka katika mafunzo wanakikundi walianza kupanda mazao ya chakula cha vipepepo (mimea yenye maua) ambayo yatavutia na kutoa chakula kwa vipepeo.

## Wakulima hufanya nini na vipepeo?

Katika mradi huu wakulima hukamata vipepeo majike na kuwaweka katika banda la kufugia/ kuzalishia lenye mimea ya chakula (mimea yenye maua). Vipepeo hutaga mayai kwenye mimea hiyo na kwa uangalifu wakulima huvuna mayai na kuyahifadhi katika vyombo salama. Ndani ya kipindi cha siku 14 mayai hayo hutotolewa na kuwa viluwiluwi wanaoitwa viwavi (caterpillars) Kisha wakulima huhamisha viwavi na kuviweka katika mimea husika yalipotagiwa mayai na huyafunika matawi ya mimea ili kuzuia viwavi visipotee. Siku 14 zinazofuata viwavi hujishikisha katika majani au matawi ya mimea na kujivua gamba la juu na kuwa mabuu (pupa). Mabuu hawa ndio ambao wakulima huvuna na kuwauza nje ya nchi kwa madalali/kampuni zilizopo katika Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani. Mabuu yanapofika nje ya nchi wanatumika katika bustani na kama mapambo kwenye maonyesho.

**Mwaka 2017 wakulima wa vipepeo walifanikiwa kuuza hadi kufikia mabuu 865 walioingiza ShT. 1,186,530 sawa na wastani wa bei ya ShT 1,371.7 kwa kila buu.**

"Watu walipokuwa wakiniona nazunguka zunguka na kineti changu kidogo kukamata vipepeo walinicheka wakihisi nina matatizo ya akili!"

**Emmanuel E. Singo**

## MSESE E. ELIFURAHA

Mwaka 2017 niliuza mabuu 330 kwa ShT 419,430. Nilizitumia fedha hizo kukarabati nyumba yangu... nimebadilisha sakafu ya zamani na kuweka marumaru (tiles) na madirisha ya kisasa [aluminiamu]. Mradi huu umewahamasisha wanakijiji wengi na kubadilisha mtazamo wao juu ya msitu, wanauheshimu msitu kwa kuwa wanajua kwamba vipepeo wanatoka msituni. Kwa hiyo, kama wataharibu misitu hawatapata vipepeo na hivyo hawatapata pesa.



## RIDI ELIAMANI

Ufugaji wa vipepeo umesaidia kuleta mwanga katika nyumba yangu, nilipata ShT 90,000 kwa kuuza mabuu na nikaamua kuzitumia fedha hizo kuweka vifaa vya umeme wa sola (solar) katika nyumba yangu. Watoto wangu walifurahi sana kusoma kwa kutumia taa za umeme, waliongeza muda wa kusoma kutoka saa moja walilokuwa wakisoma hapo awali, wakati mwingine walisoma hadi usiku wa manane.



## EMMANUEL E. SINGO

Binti yangu alisimamishwa masomo kwa sababu nilishindwa kulipa ada ya ShT 60,000 lakini baada ya kuuza mabuu 189 nilipata ShT 256,840 na kulipa ada ya shule. Binti yangu alifurahi sana kwa kuwa ilibaki kidogo tu akose mitihani yake ya mwisho.





## NAVONE EMMANUEL E. SINGO (Mwanafunzi, Binti wa Emmanuel E. Singo)

Niliona aibu sana kumwona baba yangu anakamata vipepeo lakini baadaye tuliona fedha zikipatikana kutokana na vipepeo. Sasa namsaidia kuangalia banda la vipepeo..... na ninaipenda kazi hii. Kabla baba yangu hajaanza kufuga ipepeo, nilikuwa nakosa baadhi ya masomo shuleni kwa kuwa ada ilikuwa hailipwi kwa wakati. Nakumbuka nilikuwa nabaki nyumbani kwa wiki 2-3 zaidi wakati marafiki zangu walikuwa tayari wapo shule.



# Ufugaji wa Nguruwe kwa manufaa mbalimbali

**Kijiji cha Ukwega, Wilaya ya Kilolo**
**Misitu iliyoko jirani: Hifadhi za Mazingira Asilia za Kilombero na Uzungwa Scarp**

EAMCEF ilisaidia ufugaji wa nguruwe ili kuthibitisha kama jamii inaweza kupata kipato kutoka chanzo mbadala mbali na misitu na kwa hiyo, jamii ingepunguza utegemezi wa moja kwa moja wa misitu. Kwa kufanya hivyo wangewezesha utunzaji wa bioanuwai katika Hifadhi za Mazingira Asilia za Kilombero na Uzungwa Scarp. Ufugaji wa nguruwe ulikuwa chaguo bora litakaloweza kuwa suluhisho endelevu katika kupunguza kasi ya umaskini kwa kuwa ufugaji huu una faida nyingi ambazo ni - kupata mapato yatokanayo na uuzaji nguruwe, chanzo cha protini, kupata mbolea ya samadi kwa ajili ya bustani na kuzalisha umeme wa gesi itokanayo na kinyesi. Mnamo mwaka 2013 mradi ulianza kutekeleza wazo hili kwa kutoa elimu ya kuhifadhi mazingira na kutoa mafunzo ya ufugaji wa nguruwe na baadaye kutoa 'mbegu' ya nguruwe katika vijiji vinne kwa wanavijiji 168. Ili kusambaza manufaa kwa wanavijiji wengi zaidi wanavijiji walikubaliana kushirikiana na kaya jirani ambazo hazikuwa kwenye mradi kwa kuzipatia bure mtoto mmoja wa nguruwe atakayezaliwa. Mpaka ilipofika kipindi cha kufunga awamu ya kwanza ya mradi mwaka 2016, mradi ulishuhudia mabadiliko ya hali za maisha katika kaya zilizojihusisha na mradi, pamoja na kupungua kwa kiasi kikubwa kwa idadi ya watu walioripotiwa kuvamia misitu.

**Nyama ya Nguruwe imekuwa ikipatikana kwa urahisi katika mabucha ya kijiji ukilinganisha na nyamapori ambayo ilikuwa ikipatikana kwa uwindaji haramu katika Hifadhi za Asilia kwa kuchoma nyasi ili kuwatisha wanyama lakini pia kuharibu misitu. Mapato yanayotokana na kuuza watoto wa nguruwe/nyama ya nguruwe yameboresha kipato cha familia ilihali mbolea imetumika kuboresha bustani za majumbani.**



## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka katika eneo la mradi - Wilaya ya Kilolo

- **Wanakijiji 283 (wakiwemo wanawake 149: wanaume 134)** walipewa mafunzo ya ufugaji wa nguruwe
- **Kaya 168** zilipewa mbegu bora ya nguruwe
- **Kaya 124** zilipokea watoto wa nguruwe kutoka kwenye nguruwe waliotokana na majirani zao
- **ShT 31,135,000** zilipatikana kwa kuuza nguruwe/watoto wa nguruwe
- **ShT 4,430,000** zilipatikana kutokana na uuzwaji wa nyama ya nguruwe
- **Kilo 2713** za mbolea ya nguruwe zilitumika katika bustani za majumbani

## RITHA ALMAS MGOBA



Tangu nilipoanza kutumia mbolea ya nguruwe nimeshuhudia uzalishaji ukiongezeka kiasi kwamba niliweza kuuza ziada ya mahindi na maharage na kulipia watoto wangu ada ya shule.Hapo zamani, haikuwa rahisi kuuza chakula kwa sababu mavuno yalikuwa kidogo sana. Kama mradi huu utaendelea utasaidia watu wengi, uhaini wa misitu utaisha kabisa kwa kuwa watu hawatakuwa na sababu ya kuvamia misitu.

## DISMAS WILLIAM KIGAVA



Nilishawishika kuanza kufuga nguruwe baada ya kuona maisha ya rafiki yangu yanabadilika na kuwa mazuri kila siku, nilifanya uamuzi wa kujiunga na mradi siku niliyomtembelea kwake na kushangazwa kwa kuona watoto tisa wa nguruwe waliozaliwa na nguruwe mmoja. Najiona nikiwa tajiri kufikia mwaka 2020, nitakuwa tajiri kama rafiki zangu. Naona maisha mazuri kwa siku zijazo na pia kwa ujasiri naweza kuwahamasisha watu wengine kufuga nguruwe.

## AMARIA DOMINICUS KIMATA



Nilikuwa nikigombana na mume wangu kwa kuwa nyumba yetu ilikuwa ya kizamani, tulikuwa hatulali mvua ikinyesha usiku. Sasa tuna furaha sana kwa kuhamia katika nyumba mpya tuliyoijenga kutokana na fedha za mauzo ya nguruwe – hakuna ugomvi tena! Nilichukua kiasi cha fedha za mauzo ya nguruwe na kuanzisha biashara ndogondogo hapa kijijini. Ninatengeneza mikate na maandazi na kuuza hapa kijijini ambapo hupata hadi ShT 65,000 kwa mwezi.



## FAIDA WILBERT KIHOO



Kupitia mradi huu (wa kufuga nguruwe) sasa ninaweza kujiunga na VICOBA na kupata mikopo midogomidogo. Kabla ya hapo sikuwa na fedha za kuniwezesha kufanya hivyo. Maisha yetu yalikuwa magumu sana na haikuwa rahisi kupata fedha, niliposikia habari za mradi niliamua kujiunga..... baada ya kujiunga maisha yangu yamebadilika.

## TIRNESY ASTANDI KITOSY



Niliuza nguruwe 9, nikapata ShT 700,000 nikatengeneza matofali na kujenga nyumba ya familia na kuachana na nyumba yangu ya kizamani, ambayo ni ndogo na ilikuwa inanifanya nisiwe na uhuru wa kuwa faragha na mke wangu. Kutokana na mapato yaliyotokana na nguruwe niliweza kuweka mitambo ya umemejua katika nyumba yangu. Umeme huu umempa mke wangu uhuru wa kufanya kazi usiku kucha.... anakaanga maandazi usiku na kuyauza asubuhi. Mimi pia hutumia umeme kwa kutoa huduma ya kuchajisha simu za wanakijiji wengine na kupata kipato cha ziada cha takribani ShT 15,000 kwa mwezi.



"Kutokana na mapato ya kuuza nguruwe niliweza kuweka vifaa vya umemejua katika nyumba yangu. Umeme huu umempa mke wangu uhuru wa kufanya kazi usiku kucha...anakaanga maandazi usiku"

**TIRNESY ASTANDI KITOSY, Kijiji cha Ukwega, Wilaya ya Kilolo**



# Ufugaji mbuzi wa maziwa ni tofauti na mazoea

**Kijiji cha Mkalanga, Wilaya ya Kilolo**
**Misitu ya jirani: Hifadhi za Mazingira Asilia za Uzungwa Scarp na Kilombero**

Ni watu wachache tu katika Kijiji cha Mkalanga waliamini kwamba mbuzi wanaweza kuwa chanzo kizuri cha maziwa.... kama ilivyo kwa ng'ombe na kwamba mapato yanayotokana na ufugaji wa mbuzi yanaweza kubadili maisha ya wanavijiji maskini. Ufugaji wa mbuzi wa maziwa ulionekana siyo jambo la kawaida na la ajabu kutekeleza. Kupitia ushawishi na mafunzo wanakijiji walishawishika kwamba kufuga mbuzi wa maziwa ni kitu kinachowezekana na wangalipenda kujaribu kutekeleza. Bwana Seth Chavala, mkazi wa Kijiji cha Mkalanga anaelezea simulizi yake hapa chini:

Kikundi chetu cha ufugaji wa mbuzi wa maziwa kinaitwa 'Mshikamano' wajumbe wake walichaguliwa katika mkutano mkuu wa kijiji. Mimi ni mkulima lakini naweza kusema bila kificho kwamba nimekuwa nikifaidika kidogo katika shughuli za kilimo kuliko ilivyo sasa katika ufugaji wa mbuzi. Nilianza kufuga mbuzi mwaka 2015 kupitia ufadhili wa EAMCEF, nina uhakika wa kupata lita 1.5 za maziwa kila siku ambapo huuza lita moja kwa ShT 1,000 na yanayobakia hutumiwa na familia. Hapo awali familia yangu na watu wengi katika kijiji hiki tulikuwa hatuwezi kupata maziwa kwa kuwa yalikuwa yanapatikana mbali sana na kijiji hiki na yalipatikana kwa gharama kubwa kidogo. Mapato ninayoyapata kutokana na mbuzi nayatumia kukidhi mahitaji mbalimbali ya familia, ada za shule na kununua mahitaji mengine ya kishule.

## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho katika eneo la mradi – Wilaya ya Mkinga, Manispaa ya Morogoro na Wilaya ya Kilolo.

- **Wanavijiji 314 (wanawake 154: wanaume 160)** walipewa mafunzo ya kufuga mbuzi wa maziwa
- **Wanavijiji 377 (wanawake 212: wanaume 165)** walipewa mbuzi wa maziwa
- **Kaya 108** zilipokea watoto wa mbuzi kama manufaa ya ziada ya mradi.
- **Mapato ya ShT 7,944,500** yalipatikana kwa kuuza mbuzi na maziwa.



## SETH CHAVALA

Nilikuwa na furaha sana siku niliyopokea mbuzi kutoka kwenye mradi, sasa tunafaidi sana.



## YUSTA LUHWAGO

Isingewezekana kupeleka mtoto wangu hospitali kama siyo kuwa na mradi wa mbuzi. Sina bima ya afya hivyo niliuza mbuzi mmoja na kulipa gharama za hospitali.... nina furaha kwamba sasa hivi mwanangu ni mzima. Nilianza kuuza`mbogamboga baada ya kuona kwamba naweza kupata mbolea ya samadi ya kutosha kutoka kwenye mbuzi. Mapato yanayotokana na bustani ya mbogamboga yananiwezesha kupata fedha za mahitaji ya familia. **Mbuzi wameniokoa nisiwe ombaomba na kibarua.**



## IZACK NYAMOGA


Natumia mbolea itokanayo na mbuzi katika kulima miti ya maparachichi, miti yangu ya miparachichi ina afya nzuri mno. Mwaka 2016 niliuza maparachichi na kupata ShT 210,000 kutoka kwenye miti mitatu tu. Hapo awali niliweza kuvuna maparachichi machache sana ambayo yalikuwa hayatoshi kuuza. Nimetumia fedha nilizopata kutokana na mauzo ya maparachichi kununua televisheni na kuweka umemejua nyumbani kwangu. Tangu nilipoweka umeme wa sola watoto wangu wanapata muda wa kusoma kwa muda mrefu zaidi wakati wa usiku tofauti na ilivyokuwa awali kwa kutumia taa za asili za mafuta ya taa 'kibatari'





## NELIA KIKOTI

Niliuza mbuzi mmoja kwa ShT 70,000 na kuzitumia fedha kuwalipa vibarua waliofanya kazi katika shamba langu. Nilipanda maharage na kuyauza kwa ShT 450,000. Nilitumia fedha za mauzo ya maharage kujenga nyumba kubwa ya familia. Nyumba yangu ya zamani ilikuwa ndogo sana kwa familia yangu kuenea humo.
Mbuzi wangu alipozaa (sasa nina mbuzi 7) niliuza mbuzi mmoja na kuajiri watu wa kusaidia kupanda miti katika shamba langu la ekari moja. Huwa napata lita 3 za maziwa kwa siku, kwa kawaida huuza lita mbili na kutumia maziwa yanayobaki. ....tangu wakati huo maisha yangu yamebadilika sana ninaweza kijipandisha daraja kutoka hatua ya 1 hadi ya 10 yote hii ni kutokana na ufugaji wa mbuzi.



"Niliuza maparachichi na kupata ShT 210,000 kwa miti mitatu tu...Nimetumia fedha nilizopata kutokana na mauzo ya maparachichi kununua seti ya televisheni na kuweka umeme wa sola.

**IZACK NYAMOGA, Kijiji cha Mkalanga, Wilaya ya Kilolo**



# Kama mazao ya kilimo hayatabadilisha maisha yetu, ng’ombe wa maziwa watayabadilisha

**Kijiji cha Idegenda, Wilaya ya Kilolo**
**Msitu uliopo jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Uzungwa Scarp**

Unaposikia kuhusu mradi wa kuhifadhi misitu utawaza kuhusu mambo muhimu kama vile kufanya doria katika msitu, kusafisha mipaka, na mipango ya usimamizi wa msitu. Bi. Aghata Kipingi na wenzake wameunda kikundi cha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa katika Kijiji cha Idegenda (Wilaya ya Kilolo) wanaeleza simulizi yao ya namna mradi wa kufuga ng'ombe wa maziwa uliofadhiliwa na EAMCEF ulivyobadilisha maisha yao na kupunguza utegemezi mkubwa katika misitu ili kujipatia kipato cha familia.

**Kikundi chetu chenye jumla ya watu 25 kiliundwa mwaka 2013 wakati wa Kikao chaKijiji wakati EAMCEF walipofika kijijini kwetu. Tulipata mafunzo ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na ujenzi wa mabanda mazuri ya ng'ombe. EAMCEF walitupatia ng'ombe jike9 na dume 1 kwa ajili ya kuanza mradi, kwa sasa (2017) tuna jumla ya ng'ombe 23.**

Katika nyumba yetu tulifanikiwa kuweka mtambo mdogo wa bayogesi [gesi itokanayo na kinyesi cha ng'ombe] ambao unatumia kinyesi cha wanyama kutengeneza nishati ya kupikia. Nilinunua stovu na kujenga jiko kubwa. Hapo awali nilikuwa nikitumia muda mrefu msituni hadi kufikia saa sita kutafuta kuni. Kwa kutumia bayogesi, muda niliouokoa nautumia kutunza ng'ombe na shamba langu. Kwa sasa siendi tena msituni kama hapo awali lakini pia nafurahia jiko langu lisilofuka moshi na mume wangu sasa anajisikia huru kuwa nami jikoni wakati napika. Jiko jipya limepunguza matumizi ya kuni kwa aslimia 75 hivyo kupunguza uharibifu wa misitu inayotuzunguka. Kama kaya zote katika Kijiji cha Idegenda watafuga ng'ombe na kutumia majiko ya bayogesi.... misitu inayotuzunguka [Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Uzungwa Scarp] itabakia kuwa na uzuri wake wakati wote.



## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka katika eneo la mradi-Wilaya ya Kilolo.

- **Wanakijiji 40 (wanawake 17: wanaume 23)** walipewa mafunzo ya usimamizi wa ng'ombe wa maziwa
- **Ng'ombe 20** walinunuliwa na kusambazwa kwa wanakijiji 42
- **Mapato ya ShT 53,462,200** yalikusanywa kutokana na mauzo ya maziwa
- **Kilo 15,794 za samadi ya ng'ombe** zilitumika kama mbolea
- **Kilo 10,253 za samadi ya ng'ombe** zilitumika kutengenezea bayogesi

## AGATHA KIPINGI

Kabla ya kujiunga na mradi familia yangu haikuwahi kutumia maziwa lakinisa sa napata maziwa ya ziada na kuyauza kwa wanakijiji wenzangu. Kwa miaka miwili iliyopita niliweza kupata takribani ShT 3,000,000. Nilitumia fedha zangu kununua ekari 2 za ardhi na kupanda miti 1,200 ambapo nilipata karibu ShT 6,000,000 kutokana na miti. Nilitumia baadhi ya fedha kulipa ada ya shule kwa watoto wangu watatu na kuweka maji ya bomba nyumbani kwangu. Hapo awali nilikuwa nikitafuta kuni kuanzia saa 12 Asubuhi hadi saa 5 Asubuhi na nilikuwa siwezi kushughulikia shamba langu ipasavyo. Ng'ombe wananipatia bayogesi hivyo sipotezi tena muda msituni kutafuta kuni. Muda huo nautumia kutunza ng'ombe na bustani yangu.

Kabla sijaanza kutumia mbolea ya ng'ombe nilikuwa navuna magunia matatu ya mahindi kwa heka moja lakini sasa mavuno yameongezeka mara dufu.

## SIFA MWANDILA

Kwa kutumia jiko la kupikia la bayogesi nimekuwa nikifurahia kwa sababu sipati shida kuwasha moto, hakuna moshi, hakuna masizi, jiko linakuwa safi.... na pia siku hizi naona mume wangu anafurahi kuwa jikoni. Majirani zangu wananiambia kwamba nina raha siku hizi kwa kuwa sipati tena matatizo ya kutumia jiko la asili la mafiga matatu.

## HARUNAH SIMAMBILI MOTO

Nisingeweza kulipa ada ya shule ya watoto wangu kama si fedha za kuuza maziwa. Napata ShT 700,000 kila mwezi jambo ambalo lilikuwa haliwezekani hapo awali.
Siendi tena msituni kutafuta nyama, ninauza maziwa na kupata fedha za kutosha kununua nyama katika bucha yoyote.





## Furaha ya mtambo wa bayogesi

"Katika nyumba yangu tumeweza kuweka mtambo mdogo wa bayogesi unaotumia kinyesi cha wanyama kuzalisha nishati ya umeme kwa ajili ya kupikia, nimenunua jiko la kupikia na kujenga jiko zuri"

**Sifa Mwandila wa Kijiji cha Idegenda, Wilaya yaKilolo**



# Jinsi upandaji miti unavyopindua umaskini katika Wilaya ya Kilolo

**Kijiji cha Idegenda, Wilaya ya Kilolo**
**Msitu uliopo jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Uzungwa Scarp**

Mandhari ya kuvutia ya Wilaya ya Kilolo imebarikiwa na hali ya hewa ya ubaridi na ardhi yenye rutuba inayostawisha miti vizuri hata hivyo, kwa miaka mingi changamoto kubwa imekuwa "muda wa kusubiria" muda huu ni ule wa kusubiria tangu kupanda miti hadi kuvuna. Kuuza miti iliyokomaa inahitajika kusubiri kwa takribani miaka 15 ili kufaidi mazao ya misitu- Huo ni muda mrefu sana!


Wakati wakisubiri kwa zaidi ya muongo mmoja, wanajamii wa Kijiji cha Idegenda, kijiji kimojawapo katika Wilaya ya Kilolo hujishughulisha na shughuli za kilimo na zisizo za kilimo ili kujiingizia kipato. Katika shughuli zisizo za kilimo, misitu ya Uzungwa kwa kuwa ipo jirani imekuwa siku zote ikiathirika kwa kukatwa miti (mbao na fito) na shughuli nyingine zinazosababisha uharibifu wa misitu.

Ili kutatua tatizo hilo, EAMCEF kwa kutumia mbinu shirikishi walikatisha "muda wa kusubiri" kwa kuanzisha upandaji wa miti ya misonobari (pines) inayokua haraka (miaka 7) ambayo itatumika kama chanzo mbadala cha kipato ili kuzuia uharibifu wa misitu. Mbali na kupanda miti, wanakijiji huotesha na kuuza miche hiyo ya miti.

## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka maeneo ya mradi: Wilaya za Korongwe, Mkinga, Lushoto, Morogoro, Kilolo na Manispaa ya Morogoro

- **Wanakijiji 1,049 (wanawake 514: wanaume 535)** walipewa mafunzo kuhusu mbinu za upandaji miti
- **Vitalu 299** vya miti vilianzishwa
- **Hekari 25,285** zilianzishwa kwa ajili ya upandaji miti
- **Mapato ya ShT 35,965,650** yalipatikana kwa kuuza miche ya miti.



## WILSON MGATA (Mwenyekiti wa Kijiji)



Mwaka 2013 nilipanda miti 3,600 katika shamba la heka 6. Ninatarajia kwa furaha kupata ShT 60,000,000 ndani ya kipindi cha miaka 2-3 ijayo kwa kuuza miti. Nimefurahishwa sana na huu mradi. Tayari nimepata ShT 35,000,000 kwa kuuza miche ya miti kama mbegu. Nilitumia baadhi ya fedha kujenga nyumba ya biashara ambapo huwa napata ShT 140,000 kwa mwezi. Natumia fedha hizi kukidhi mahitaji yangu yote ya nyumbani na pia nimejenga nyumba ya kisasa kama zile zinazoonekana huko mjini.

Hapo zamani tulikuwa tunashuhudia mioto ikiwaka msituni hadi mara mbili kwa wiki lakini sasa hakuna matukio ya moto tena kwa sababu wanakijiji muda mwingi wanashughulikia miti yao.

## EXAVERY SAMIGARI KISIMBA



Nimekuwa nikipanda miti kwa miaka 30 sasa lakini nilishangaa kusikia kutoka kwa EAMCEF kwamba kuna aina ya miti ambayo hukua kwa muda mfupi. Bila kuchelewa nilianza kuipanda na kuuza miche ya miti ambapo nilipata takribani ShT 20,000,000 kwa kipindi cha miaka mitatu na baadaye nilipanda heka 20 za shamba langu mwenyewe. Nilitumia baadhi ya mapato ya kuuza miche ya miti kujenga nyumba ya kisasa katika mji wa Iringa hivyo kuokoa fedha ambazo mimi na familia yangu pamoja na ndugu tungezitumia kulala katika nyumba za wageni kipindi tunapokuwa Iringa.

Fedha zilizopatikana kwa kuuza miche ya miti ziliokoa uhusiano kati yangu na mke wangu... kila mara tulipohitaji kuwa na faragha ilitulazimu kwenda mbali na nyumbani kwa kuwa nyumba yetu ilikuwa ndogo na watoto wakiwemo unaweza ukapata picha ni kwa vipi ilikuwa vigumu kufurahia na mke wangu! Wakati mwingine tulisubiri mpaka usiku wa manane.




## MBAWI PRIMARY SCHOOL, KILOLO DISTRICT

Mradi wa kupanda miti umeisaidia shule kutatua changamoto za muda mrefu hasa zinazohusiana na huduma zinazotolewa kwa wanafunzi. Mapato yaliyotokana na kuuza miche ya miti yalitumika kujenga jiko kubwa, kununua vifaa vya kupikia na kupakulia n.k. lakini jambo la muhimu zaidi ilikuwa kuweka umeme wa sola ili kusaidia wanafunzi ambao wanasubiri mtihani wa taifa wa darasa la saba kupata muda wa ziada kujisomea wakati wa usiku. Walimu wanaamini kwamba umeme wa sola umechangia katika matokeo mazuri ya wanafunzi ambapo walifaulu kutoka 60.3% (mwaka 2016) hadi 68.9% (mwaka 2017). Alieleza Ponziano Lung'ali (Mwalimu wa Mazingira, Shule ya Msingi Mbawi, Wilaya ya Kilolo).



Mapato kutokana na mauzo ya miche ya miti yalitumika kujenga jiko kubwa, kununua vifaa vya kupikia na kupakulia n.k.

**Shule ya Msingi Mbawi, Wilaya ya Kilolo**



“Shule yetu ilikuwa na vikombe vichache sana kiasi kwamba wanafunzi wengi walilazimika kunywa uji kwa makundi, wale wenye vikombe walitakiwa kunywa uji haraka na kuwapatia wenzao vikombe. Uji ulikuwa hauna sukari lakini kwa sasa sukari si tatizo tena”

**Seth Madembo (Mwanafunzi, Shule ya Msingi Mbawi, Wilaya ya Kilolo)**



# Kama isingekuwa ufugaji...

**Kijiji cha Msufini, Wilaya ya Kilombero**
**Msitu uliopo jirani: Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa**

Wanakijiji wa Kijiji cha Msufini, Wilaya ya Kilombero wanaoishi chini kabisa ya Mlima Udzungwa, wanafurahia mwonekano mzuri wa msitu na mandhari iliyo jirani nao. Katika kijiji hiki EAMCEF ilichagua kikundi kidogo cha wakulima kuonyesha kwa vipi ufugaji nyuki kwa kutumia mizinga ya kisasa unaweza kuwa shughuli yenye faida kiuchumi ambayo itabadilisha maisha ya watu na kuwapa njia mbadala ya kuingiza kipato na kuwa kama motisha itakayowaepusha kujitafutia kipato kwa kuvamia misitu iliyohifadhiwa. Miaka kumi iliyopita kabla ya mradi wa EAMCEF, kikundi cha wakulima 10, kati yao wanaume walikuwa 6 waliunda kikundi cha kufuga nyuki kilichoitwa "Wosia wa Baba". Kikundi kilitengeneza mizinga ya asili 10 ambayo hutengenezwa kwa magogo a kuining'inizwa kwenye miti msituni ambao ni msitu wa hifadhi. Kila mzinga ulizalisha asali kiasi cha lita 5 tu kwa mwaka. Kwa hiyo, kikundi kilizalisha takribani ShT 50,000 hadi 60,000 kwa mwaka.

Kikundi hakikuwa na vifaa vyovyote vya kurinia asali. Wakati wa kuvuna asali kwa kawaida wafugaji huwasha moto ili kuwakimbiza nyuki. Katika mchakato huo moto huwa haudhibitiwi na husambaa katika miti iliyokaribu na wakati mwingine huenda mbali zaidi katika msitu. Mamlaka zinazohusika na misitu katika eneo hilo zilizuia shughuli hizo na kuweka hatua madhubuti za kuzuia watu kuharibu misitu. Kikundi hicho kikawa miongoni mwa waathirika walioachwa bila kuwa na shughuli mbadala zaidi ya kuning'iniza mizinga katika miti iliyo karibu na kijiji. Kikundi kiliamua kuchaguaeneo dogo na kulipanda miti ili kuendelea naufugaji lakini kiuchumi shughuli hii haikuwa yenye manufaa.

**Ili Kuufanya ufugaji nyuki kuwa biashara yenye faida** ambayo itawaondoa wanakijiji katika uvamizi wa misitu iliyohifadhiwa, EAMCEF iliingilia kati na kutumia fursa ya kikundi kilichokuwapo kuanzisha mbinu mpya za ufugaji wa nyuki.

## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka maeneo yote ya mradi – Wilaya za Korogwe, Mkinga, Lushoto, Same, Morogoro, Kilombero, Mvomero, Kilolo na Mufindi

- **Wanakijiji 1,570 (wanawake 680: wanaume 890)** walipewa mafunzo kuhusu mbinu za kisasa za ufugaji nyuki
- **Vikundi 82** vya ufugaji nyuki viliundwa
- **Mizinga ya kisasa 1,352** ilisambazwa kwa wanakijiji/vikundi
- **Lita 14,180** za asali zilivunwa
- **Kilo 508 za nta** zilikusanywa
- **Mapato ya ShT 76,647,400** yalikusanywa kutokana na mauzo ya asali na nta



## GODFREY DANIEL HORO (Mwenyekiti wa Kikundi cha Wosia wa Baba)

Mwaka 2016 pekee tulipokea mizinga ya kisasa 50 kutoka EAMCEF, kila mzinga ulizalisha lita 15-20 za asali mara tano zaidi ya kiasi tulichokuwa tukivuna kutoka kwenye mizinga ya asili. Mwaka 2016 pekee tuliuza lita 250 za asali kwa ShT 2,500,000 na kutumia kiasi cha fedha hizo kukodisha ekari mbili za shamba na ambalo tulilima miwa.

Kutokana na kilimo cha miwa tulipata ShT 2,500,000 na kutumia kiasi cha fedha hizo kuanzisha biashara nyingine - Tulinunua baiskeli 10 na kuzikodisha kwa ajili ya huduma za usafiri kijijini. Kwa baiskeli hizo tulipata ShT 5,000,000 ndani ya kipindi cha miezi 6.

Kila mwanakikundi alipokea gawio la 25%, nilitumia fedha yangu kumnunulia baiskeli mwanangu ambaye alikuwa akitembea Km 14 kila siku kwenda shule. Kwa kutumia baiskeli hiyo mwanangu anaweza kurudi nyumbani mapema na kufanya kazi zake za shule.... katika mitihani yake sasa anapata alama ya 70-80% tofauti na ya awali ya 50-55%.

Mafanikio yetu kama kikundi yamechangia kuundwa kwa vikundi vingine 15vya ufugaji wa nyuki katika kijiji hiki. Wanakijiji hawahatarishi tena maisha yao kwa kwenda msituni kutafuta kipato.

**Kikundi chetu kimefanya mabadiliko makubwa kijijini, tunakopesha fedha kwa watu wenye uhitaji mkubwa hasa katika VICOBA bila kuwatoza riba. Kikundi chetu kimeokoa maisha ya wanakijiji 4 ambao walikuwa wanaumwa sana ila hawakukuweza kumudu gharama za matibabu.**




## RAJAB MOHAMED MALIPA


Sisi [Kikundi chetu] ni kama wahifadhi misitu, kwa kujishughulisha na ufugaji wa nyuki tunajua kwamba nyuki wanategemea mazingira yanayotuzunguka hivyo haturuhusu mtu yeyote kukata miti au kuichoma..... nina hamasa kubwa na huu mradi na sasa ni mwalimu mzuri wa wanajamii wengine. Ningependa kuwashauri wanakijiji kuhakikisha kwamba wakati wa zoezi la kupanga matumizi ya ardhi ya kijiji sehemu kubwa ya ardhi itengwe kwa ajili ya kupanda miti pamoja na shughuli za ufugaji nyuki. Hii itasaidia kupunguza kasi ya uharibifu wa misitu ya hifadhi kwa kuwa misitu ya kupandwa inaweza pia kuwapatia wanakijiji kuni.

## RECKSON ARON MTAMA (Katibu wa Kikundi cha Wosia wa Baba)

Nyuki (akimaanisha ufugaji nyuki) wanatosha, nakumbuka nilinusurika kugongwa na mamba [akimaanisha nyoka] nikiwa natafuta asali katika msitu. Sihitaji tena kwenda msituni. Kwa sasa sina wasiwasi kuhusu kulipa ada ya wanangu, hapo awali nilikuwa naaibisha.... niliwahi kukopa ShT 40, 000 kwa ajili ya kulipa ada lakini niliishia kulipa gunia moja la mpunga lenye thamani ya ShT 100,000!

## HIDAYA SAID MATAJIRI

Mimi ni mwanamke mjane lakini sina wasiwasi kwa sababu ninatumia mapato yanayotokana na ufugaji nyuki kuwekeza katika shughuli nyingine za uzalishaji. Mwaka jana sikushika jembe kabisa, badala yake nilikodisha trekta likalima shamba langu.



# Malipo ya ahadi ya kuhifadhi misitu

**Shule ya Msingi Kazita, Wilaya ya Muheza**
**Msitu ulioko jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Nilo**

Je, wanajamii wa Kazita watatekeleza ahadi yao ya kutunza msitu wa Asili wa Nilo uliopo jirani nao? Simulizi ya Shule ya Msingi inaeleza kila kitu.

## Wakati wa ufunguzi wa shule mwaka 2008


Shule ilikuwa na vyumba viwili kimoja kilifanywa darasa na kingine ofisi ya jumla ya walimu na watoto wa darasa la awali. Darasa moja liligawanywa kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili. Ugawanyaji ulifanywa kiasi kwamba wanafunzi wa madarasa hayo mawili walikaa wakielekea pande mbili tofauti (wakipeana mgongo). Darasa moja lililazimika kuwa katika hali ya ukimya huku wanafunzi wakiamrishwa kulaza vichwa vyao kwenye madawati ikiwa mwalimu alikuwa anafundisha wanafunzi wa darasa jingine waliokaa kuelekea upande mwingine ndani ya darasa hilo hilo moja. Lakini jambo hili halikuwa rahisi kama inavyosomeka kwenye maandishi haya. Ofisi ya jumla ya walimu ilimjumuisha mwalimu mkuu, msaidizi wa mwalimu mkuu na walimu wengine.

## Ufadhili wa EAMCEF

Kama mkakati wa kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Misitu ambao ni ushirikishwaji mkubwa wa wanajamii katika kusimamia misitu inayomilikiwa na serikali katika Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Msitu wa Nilo, EAMCEF ilianzisha mazungumzo na mikutano ya kushauriana na wanakijiji wa Kijiji cha Kazita kuhusu njia zitakazowezesha ushirikishwaji wa kikamilifu wa wanajamii katika shughuli za usimamizi wa misitu.

Kwa kuwa mbinu ya EAMCEF ya usimamizi wa misitu ni kwa kupitia usaidizi katika shughuli za maendeleo ya jamii, makubaliano yalifanywa kupitia kikao cha Kijiji ya kusaidia wanajamii kujengea shule vyumba vitatu (viwili vya madarasa na kimoja cha ofisi) ili kufidia nguvu na muda ambao wanajamii wanatumia katika shughuli za uangalizi wa msitu kupitia kamati zao. Kabla ya ufadhili wa EAMCEF, wanajamii walikuwa wakiingia msituni ili kujipatia mazao ya miti/mbao ambayo yaliwawezesha kujipatia fedha ya ziada ili kutimiza ahadi zao za michango ya ujenzi wa shule/madarasa.

Tangu EAMCEF ichukue jukumu hilo wanajamii walisitisha kutoa michango ya fedha ila walipaswa kufidia kwa kushiriki katika kutunza misitu. Kutokana na ufadhili wa EAMCEF shule iliongeza uandikishaji wa wanafunzi wapya.



### TAKWIMU MUHIMU

- **Madarasa mapya 2** yalijengwa
- **Ofisi 1 ya walimu** ilijengwa

## OMARI IDDI MWANGIA (Msaidizi wa Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi Kazita)

Mazingira ya kufanyia kazi kwa sasa ni mazuri, mwalimu mkuu ana ofisi yake mwenyewe, wanafunzi pia wana vyumba vyao wenyewe. Tumeshuhudia ufaulu wa wanafunzi ukibadilika tangu tuanze mradi. Msitu pia uko salama kwa sasa kwa kuwa wazazi hawavamii tena ili kujipatia fedha.






## ADAM BAKARI MBIU (Katibu, Kamati ya Ujezi wa Shule)

Mradi huu umewahamasisha wanakijiji kutunza msitu wa Nilo, wanakijiji waliunda kamati ya mazingira na kushiriki kikamilifu katika kufanya doria mara moja kwa wiki. Hapo awali tulikuwa tunafanya doria mara moja kwa mwezi au hatufanyi kabisa.

Tulikuwa na furaha sana kuona EAMCEF wakisaidia ujenzi wa shule. Kupitia elimu ya uhifadhi iliyotolewa na EAMCEF, kila mwanakijiji sasa ni mhifadhi wa misitu.





# Kuokoa misitu kwa kupamabana na hali ya ukosefu wa chakula

**Kijiji cha Mbomole, Wilaya ya Muheza**
**Msitu ulioko jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Nilo**

EAMCEF waliamini kwamba, ikiwa wanajamii wa Kijiji cha Mbomole (Wilaya ya Muheza) watakuwa na uhakika wa chakula, uharibifu wa misitu utakuwa mdogo ila wasipokuwa na uhakika wa chakula uharibifu wa misitu utakuwa mkubwa. Kutokuwa na uhakika wa chakula kunasababisha wanakijiji kuvamia misitu ili kutafuta mbao za biashara, fito na nyamapori ili waweze kununua chakula cha familia zao au kulipa ada ya shule. Katika kijiji hiki hali ya kukosa uhakika wa chakula inasababishwa na upatikanaji wa mavuno duni unaosababishwa na mbinu duni za kilimo katika maeneo yenye miteremko.

Kwa kuwa ardhi ya mteremko haiwezi kuhifadhi maji kwa muda mrefu mazao mengi hufa, udongo wenye rutuba huchukuliwa na maji, mmomonyoko wa ardhi huharibu mazao na kusababisha mavuno machache na kutokuwa na uhakika wa chakula. Katika hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula misitu inakuwa mwathirika mkubwa kwa kuwa inatumiwa kama chazo kisicho na gharama cha mapato. EAMCEF iliingilia kati na kuanzisha mbinu ya kutunza udongo na maji kwa kutumia kilimo cha makinga maji.

## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka eneo lote la mradi-Wilaya ya Muheza na Manispaa ya Morogoro.

- **Wanakijiji 329 (wanawake 190: wanaume 139)** walipewa mafunzo ya mbinu za uhifadhi wa udongo na maji.
- **Kaya 106** zilitumia mbinu hizo za uhifadhi wa udongo na maji.
- **Hekta 863 za ardhi** ziliingizwa katika mradi wa mbinu za kilimo ha uhifadhi wa udongo na maji.



### DAINESS ABRAHAM MLOWE

"Kabla ya kuanza kutumia mbinu hii, shughuli ya kilimo ilikuwa ni upotezaji wa muda tu lakini sasa ni shughuli yenye faida. Kabla ya mradi nilikuwa navuna kilo 10 za maharage lakini mwaka uliopita (2016) nilivuna kilo 80 katika eneo hilohilo.

### SOPHIA CYPRIAN

"Kupitia mbinu hii nimeweza kuanzisha biashara nyingine ndogo....nilinunua kuku na sasa nauza mayai. Napata fedha za kutosha kulipa ada ya shule.



## MICHAEL SIMON

Kwa kutumia mbinu hii ya kilimo cha makinga maji, sasa inawezekana kupanda mbogamboga katika shamba langu. Kwa mfano, mwaka 2016 nilivuna hadi Kilo 500 za mbogamboga. Baada ya kuuza nilipata ShT 800,000 na nilizitumia fedha hizo kuongeza shamba langu kutoka ekari 1 hadi 4 na pia nilichimba ambacho napanga kukitumia kumwagilia.

## JOHN LENGE

Kabla sijaanza kilimo cha makinga maji mavuno yangu hayakuwa zaidi ya magunia 2 [kilo 200) lakini inashangaza kuona napata mavuno ya magunia 7 kutoka katika shamba hilohilo. Nilikuwa na chakula cha kutosha mwaka uliopita [2016], niliuza mavuno ya ziada na kununua ng'ombe.



## HASHIM SALEHE POMBEKALI

Kilimo cha makinga maji kilianzishwa katika kikundi chetu cha kilimo kinachoitwa ANGAZIA... tulifurahi kuona mavuno yanaongezeka kiasi cha kuweza kukidhi mahitaji ya chakula ya familia kwa mwaka mzima. Hapo awali mavuno ya mahindi yalikuwa na uwezo wa kuilisha familia kwa takribani mwezi mmoja tu. Kabla ya kuanza kutumia mbinu hii nilikuwa siwezi kulima kilimo mseto kwa kuwa baadhi ya mazao yalihitaji maji ya kutosha ili yakue. Siku hizi nachanganya mahindi, migomba na mihogo na mazao yote yanakua vizuri. Familia yangu sasa ina uhakika wa chakula. Nimewasaidia wanakijiji wengi kutumia hii mbinu bila malipo. Nakwenda katika maeneo yao kuwafundisha bure na kwa hakika najisikia furaha sana.




# Kufidia nguvu na muda wa wanajamii

Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani - Mkoa wa Tanga

Tofauti na ilivyo kwa mapori ya hifadhi ambapo shughuli za matumizi ya wanyamapori huzalisha mapato muhimu kutokana na uwindaji, Hifadhi za Asilia huzalisha mapato kwa kupitia utalii wa kupiga picha na shughuli nyingine zisizo uchukuzi wa wanyama.

Utekelezaji wa Miradi ya Usimamizi wa Maeneo yaliyohifadhiwa na Mabadiliko ya Tabia nchi uliratibiwa na kusimamiwa na wafanyakazi katika kila eneo la hifadhi lililolengwa na mradi. Shughuli za mradi zinazohusiana na usimamizi wa misitu zilifanywa kwa kushirikiana na vibarua ambao ni wanajamii wanaozunguka eneo la mradi waliochaguliwa katika mkutano wa kijiji.

Shughuli kubwa zilizoajiri wanakijiji wengi ni pamoja na: usafishaji wa mipaka ya msitu, kupanda miche ya miti pembezoni mwa mpaka wa msitu, utengenezaji wa mitaro mipya, kushiriki katika kufanya doria ya msitu, ukarabati wa maeneo yaliyoharibiwa kwauchimbaji wa madini, uanzishaji na usimamizi wa njia za asili, uanzishaji na usimamizi wa kambi pamoja na uanzishaji na usimamizi wa njia za magari ya kutembezea watalii.

Kwa kupitia washirika wake, EAMCEF iliwalipa wanajamii kwa ushiriki wao katika shughuli za usimamizi wa misitu kama namnambadala ya kupunguza gharama badala ya kuajiri kampuni ambayo ingefanya shughuli hizo kwa gharama za juu - pamoja na kwamba hapakufanyika makadirio yoyote kulinganisha ni gharama kiasi gani ya muda na fedha ingalitumika kuajiri kampuni binafsi. Ulipaji wa wanajamii ulichukuliwa kama fidia ya muda na nguvu lakini pia kama faida inayotokana na ushiriki wao katika usimamizi wa maeneo ya hifadhi. Fidia ilifanyika kwa kulipa fedha taslimu kwa viwango vya serikali.Kwa ujumla kwa kipindi cha utekelezaji wa mradi wanajamii 10,800 (wanaume na wanawake) waliajiriwa na kulipwa jumla ya ShT milioni 367 kama fidia ya nguvu zao na muda wao. Kuwaajiri wanajamii wanaozunguka maeneo ya hifadhi si tu kwamba ni nafuu bali pia kunasaidia kubadilisha mtazamo wa wanajamii hasa wale ambao bado wana mtazamo wa kihistoria ambapo mbinu za uhifadhi hazikuwa shirikishi na ziliwatenga wanajamii kwa 'kingo na faini'

## Mfano kutoka Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani:

Ili kuunga mkono biashara ya utalii na usimamizi wa msitu EAMCEF ulifadhili Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani kusafisha njia za asili za msituni ambazo zitaruhusu watalii kutembea na kuzunguka katika msitu ili kufurahia mandhari ya asili ya vivutio tofautitofauti. Ufadhili huu ulilenga kutangaza hifadhi na kuhamasisha ushiriki wa wanajamii katika usimamizi wa shughuli za misitu na kuongeza kipato ambacho kitaelekezwa kwa vijiji vinavyozunguka msitu. Mbali na kupata mapato kutokana na utalii wa kiikolojia, kiasi hicho kidogo cha malipo (kama fidia ya muda na nguvu) ambacho wanajamii wanapokea kwa kushiriki katika kusafisha mipaka na njia za asili, kufanya doria ni motisha kwa wanajamii ya kuendelea kutunza misitu.



### ISAACK MATUNDA (Msimamizi Utafiti, Utalii wa Kiikolojia, Hifadhi wa Mazingira Asilia ya Amani)

Kabla ya ufadhili wa EAMCEF hatukuwahi kuwa na bajeti ya kutosha kwa ajili ya kusafisha mipaka, tulikuwa na uwezo wa kusafisha eneo dogo tu. Ufadhili wa EAMCEF umewezesha kusafisha hadi urefu wa kufikia KM 6 za njia za asili ambazo kwa sasa zinatumiwa na watalii kufikia vivutio vya kipekee, na hasahasa vinyonga na vyura wa usiku. Kutokana na msaada wa EAMCEF kumekuwa na ongezeko la watalii - kwa mfano mwaka 2014/15 watalii walikuwa 153, mwaka 2015/16 walikuwa 635 na kufikia Novemba 2017 walikuwa 763... ongezeko hili linaenda sambamba na ongezeko la mapato. Ufadhili wa EAMCEF umeongeza kujulikana kwetu katika ngazi ya taifa na kimataifa. Awali dhamira yetu ilikuwa ni uhifadhi wa misitu tu ili iendelee kutoa huduma ya maji na tulijitangaza kidogo sana, lakini kupitia EAMCEF tuliweza kuandaa taarifa za mawasiliano, programu za televisheni na redio. Msaada huu umewezesha ushirikishwaji wa karibu wa wanajamii katika shughuli za usimamizi wa misitu. Kwa kawaida tunawaajiri wanajamii kutoka katika vijiji 20 vinavyotuzunguka ili waweze kusaidia katika usafishaji wa njia za asili, tunawalipa fedha kidogo kama fidia [ya nguvu na muda wao]. Ingekuwa ni gharama kubwa sana kama tungehitaji kuajiri watu kutoka nje ya mkoa kufanya shughuli hizi.

Kupitia msaada huu tulitoa mafunzo kwa waongoza watalii wanajamii kutoka vijiji inavyozunguka ambapo mwongoza watalii anapata 60% ya ada ya kuongoza watalii, 20% inaenda kwenye serikali za vijiji husika na 20% inayobakia hubakizwa katika Hifadhi ya Mazingira Asili ya Amani. Wanajamii hushiriki kikamilifu katika doria za msituni kupitia kamati zao za mazingira, fedha kidogo zinazotolewa kwa ajili ya kufanya doria huhamasisha na kuendeleza ushirikiano kutoka kwa wanajamii na hivyo kupunguza uwepo wa shughuli zisizo ruhusiwa katika maeneo ya hifadhi.



## TAKWIMU MUHIMU

AKatika Hifadhi tisa za Asili katika Milima ya Tao la Mashariki, ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa.

- **KM 1,500 za mipaka ya misitu** zimesafishwa
- **KM 265 za mipaka ya misitu** zimepandwa miti
- **KM 199 za mipaka ya msitu** zimepimwa/zimepimwa upya
- **KM 716.10 za njia za magari** zimeanzishwa
- **KM 177 za njia za magari** za kutembezea watalii zimeanzishwa
- **Wanakijiji 10,000 na zaidi (30% wanawake)** walishiriki katika shughuli mbalimbali za kusimamia misitu.
- **Zaidi yaShT 367,000,000 z**imelipwa kama fidia ya nguvu na muda kwa wanajamii waliojishughulisha na shughuli mbalimbali za usimamizi wa misitu
- **ShT 79,853,000** zimepatikana kutokana na faini za wavamizi wa misitu pamoja na makosa mengine





# Utengenezaji wa majiko bora yenye manufaa kwa wanawake na misitu

**Kijiji cha Mbakweni, Wilaya ya Same**
**Msitu ulioko jirani: Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Chome**

Mojawapo ya swali gumu katika kushughulikia vyanzo vya uharibifu wa misitu Tanzania ni namna ya kupambana na mahitaji makubwa yanayoongezeka ya nishati ya kuni hasa katika mazingira ya kijijini ambapo 100% ya wanajamii hutegemea kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia. Ili kushughulikia changamoto hii EAMCEF ilitoa ruzuku kwa shirika lisilo la kiserikali ili kutekeleza mradi wa kuwawezesha wanawake ambao utapunguza matumizi ya kuni lakini wenye faida mbalimbali kwa vikundi vya wanawake.

## Katika Kijiji cha Mbakweni

Kijiji hiki ni miongoni mwa vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Msitu wa Chome ambapo mradi ulitoa mafunzo kwa kikundi cha wanawake - kinachoitwa Mkombozi, ya kutengeneza majiko bora ya kupikia ambayo si tu yatatumika kama mbadala wa majiko ya asili ya mafiga matatu bali pia yatakayopunguza matumizi ya kuni kwa 50% na kupunguza athari za kiafya zinazotokana na moshi jikoni. Kwa sasa kikundi kimetoa mafunzo kwa wanawake wengine na kutengeneza majiko bora 406 katika kaya tofautitofauti.

## TAKWIMU MUHIMU

Majumuisho kutoka maeneo ya mradi: Wilaya za Korogwe, Muheza, Mkinga, Same, Mvomero na Manispaa ya Morogoro

- **Wanakijiji 1,531 (wanawake 849: wanaume 682)** walipewa mafunzo ya kutengeneza majiko banifu ya kupikia yanayookoa kuni.
- **Jumla ya kaya 14,016** za Wilaya ya Mvomero, Manispaa ya Morogoro na katika Wilaya za Same, Mkinga, Muheza na Korogwe zinatumia majiko banifu kupikia.
- **Matumizi** ya kuni yamepungua kwa **50%**



## MARY AGNES

Tulikuwa katika hatari kubwa sana kutokana na majiko yetu ya kizamani kutoa moshi mwingi sana, macho na mioyo yetu ilikuwa ikiumia. Majiko haya yalikuwa yanachafua sana jiko na kufanya lisivutie. Familia yangu imekuwa ikitumia kati ya saa 24-32 kwa wiki kutafuta kuni kiasi kwamba hatukuweza kufanya shughuli nyingine zozote baada ya kutoka kutafuta kuni msituni. Tumeweza kupunguza matumizi ya kuni kwa 50% kwa kutumia majiko haya mapya, tunapika kwa urahisi, usafi, usalama na tunatumia muda mfupi sana.






## MARY BARUBUKA

Nilikuwa nikigharimia ShT 10,000 kwa wiki kwa ajili ya kuni lakini kwa kutumia majiko haya mapya sasa natumia ShT 4,000 kwa wiki. Natumia fedha zinazobaki kuboresha mlo wa familia.

## NIGHENJIJWE KODA

Mume wangu amefurahi sana kuniona natumia jiko la Mkombozi (jiko sanifu) hana kikwazo chochote tena kuingia nami jikoni, haikuwahi kuwa hivi hapo kabla!

## Kuhusu EAMCEF

Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki, yaani Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund (EAMCEF) ni mfuko wa udhamini ulioanzishwa na unaofanya kazi kama mkakati wa muda mrefu na wa uhakika wa ufadhili wa maendeleo ya jamii, tafiti za uhifadhi na kuendeleza bioanuwai, huduma za kiikolojia na matumizi endelevu ya maliasili katika Milima ya Tao la Mashariki iliyoko nchini Tanzania. Tasisi ya EAMCEF ilisajiliwa rasmi nchini Tanzania mnamo tarehe 6 Juni 2001 na inaendeshwa kama asasi isiyo ya kiserikali, isiyolenga katika kujizalishia faida.

## Dira

Dira yetu ni kuona kuwa Milima ya Tao la Mashariki na watu wanaotegemea milima hiyo vinaishi katika hali ya amani kama mfumo mmoja wa kiikolojia ulio endelevu. Misitu na milima itatoa mazao yake na huduma mbalimbali – kutoka maji mpaka kuwa umeme, kutoka chakula na mazao ya biashara mpaka madawa – kwa ajili ya watu wa Tanzania. Na jamii ya ulimwengu inanufaika kwa uwepo wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya bioanuwai na hifadhi kubwa ya kaboni inayopunguza ongezeko la joto la dunia.

## Dhima

Dhima yetu ni kuwezesha upatikanaji wa rasilimali ili kusaidia uhifadhi wa bioanuwai za misitu katika Tao la Milima ya Mashariki iliyopo upande wa Tanzania kupitia uwekezaji katika maendeleo ya jamii na uboreshaji wa hali za maisha, ufadhili wa kudumu kwa ajili ya usimamizi wa maeneo ya hifadhi na msaada wa kifedha kwa ajili ya tafiti za bionuwai na mabadiliko ya tabianchi.

## Milima ya Tao la Mashariki iliyopo Tanzania

Milima ya Tao la Mashariki iliyopo Tanzania imesambaa katika eneo la Kilomita za mraba takribani 5,350. Bloku kuu za Tao la Mashariki zimesambaa katika zaidi ya Wilaya kumi na tano za mikoa mitano ya Tanzania, ambayo ni; Tanga (Bloku ya Usambara Mashariki na Magharibi, na Milima ya Nguu), Kilimanjaro (milima ya Kaskazini na Kusini Upare), Morogoro (Milima ya Nguru, Uluguru, Ukaguru, Udzungwa, malundwe, Mahenge na Rubeho), Dodoma (Milima ya Rubeho) na Iringa (Milima ya Udzungwa).

## Maeneo Makuu ya kazi

1. Uhifadhi shirikishi wa jamii na shughuli za maendeleo kwa ajili ya kuboresha maisha ya jamii za vijijini zinazoishi pembezoni mwa maeneo ya misitu.
2. Tafiti za bioanuwai zinazofaa kwa ajili ya uhifadhi wa bioanuwai katika baadhi ya Milima ya Tao la Mashariki
3. Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi na Mabadiliko ya Tabianchi ili kuboresha shughuli za kiikolojia na kuimarisha uwezo wa taasis husika katika usimamizi.

Andiko hili limeandaliwa kutoka kwenye Mradi wa Kuboresha Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki iliyoko upande wa Tanzania 'Improving Conservation of the Eastern Arc Mountains of Tanzania' (2011-2016), uliofadhiliwa na Serikali ya Norway

**Mawasiliano:**

Sekretarieti ya Mfuko wa Uhifadhi
wa Milima ya Tao la Mashariki,
Kitalu Na. 348, Eneo la Forest Hill,
Barabara ya Kingalu,
S.L.P 6053,
Morogoro, TANZANIA

+255 23 293 4274
+255 23 293 4273
+255 755 330 558

eamcef@easternarc.or.tz
www.easternarc.or.tz